KUHASI NA KUONDOA KIZAZI

Kama hupendi paka wako kuzaana basi ni vemba akahasiwa, kwa kuondoa korodani (dume) na kuondoa mfuko wa uzazi (jike). Paka dume asiyehasiwa huenda mbali na hupotea nyumbani kwa muda mrefu, na akirudi huwa na vidonda kutokana na ugomvi. Paka hawa pia husambaza mkojo ili kuonyesha himaya yao na hivyo kusababisha harufu mbaya. Kwa ujumla paka dume aliyehasiwa huishi maisha marefu zaidi.

Paka jike ambaye hajaondolewa kizazi ataingia kwenye mzunguko wake kila mara, na kama hafungiwi ndani anaweza kupata mimba. Paka jike anapokuwa kwenye joto hupiga kelele sana na kuvutia madume mengi. Paka jike anaweza kuzaa mara nne (4) kwa mwaka na mzao mmoja unaweza kuwa na vitoto hadi nane (8).

Daktari wa mifugo atakushauri lini paka wako anaweza kufanyiwa upasuaji kuondoa uzazi. Paka hupona haraka baada ya upasuaji. Unaweza kumchukua paka wako siku ile ile au kesho yake baada ya upasuaji. Hata hivyo baada ya upasuaji paka apumzishwe ili apone haraka

.

DALILI ZA KUANGALIA KAMA PAKA ANAUMWA

1. Ulaji . Kama paka hali wala kunywa chakula ali-chokizoea.
2. Kama macho ni machafu na yanatongotongo, au ni mekundu na yanatoa machozi.
3. Ngozi na manyoya: kama ngozi na manyoya ya paka vimebadilika.
4. Kuvimba tumbo kusiko kwa kawaida
5. Kupumua kwa shida
6. Kuharisha au kutapika kusikosimama.

Imetolewa na
Kliniki ya Mifugo,
Kitivo cha Tiba ya Mifugo
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
P. O. Box 3015 Chuo Kikuu MOROGORO
Simu:0232 60 1495

SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE

VETERINARY CLINIC

AFYA NA MATUNZO BORA YA PAKA

YALIYOMO:

1. Huduma ya kwanza
2. Mganga wa mifugo
3. Chanjo dhidi ya magonjwa
4. Kuua minyoo
5. Viroboto
6. Kuhasi
7. Dalili za paka Kuugua

UTANGULIZI

Paka anaweza kuishi kati ya miaka 10 hadi 15 au zaidi ili mradi unamkinga dhidi ya ajali na magonjwa. Unaweza kuongeza umri wa kuishi wa paka wako kwa kumjali kumtunza vizuri na kumpa mahitaji muhimu katika maisha yake. Paka anahitaji mlo uliokamili ili kumfanya awe mwenye afya, lakini pia anahitaji hifadhi na upendo ili awe mwenye furaha.

HUDUMA YA KWANZA

Paka anapoathirika kwa namna yoyote ile mwone Daktari wa mifugo. Hakikisha unajua namba ya simu ya Daktari wa mifugo, muda wa kazi na taratibu za kupata huduma za dharura. Matatizo yanayoweza kumpata paka wako ni kama vile ajali, kula sumu na magonjwa

Si rahisi kila mara Daktari wa mifugo kuja nyumbani kwako kumwona paka wako, hivyo ni bora kama utampeleka kliniki ambako ataweza kupata huduma iliyo kamili.

Kikapu au boksi la kubebea paka ni muhimu kila unapompeleka paka wako kliniki. Hii itamzuia kutoroka, kugombana na paka wengine au mbwa na pia kupunguza uwezekano wa kuambukizwa magonjwa. Hakikisha kapu au boksi linapitisha hewa pia weka magazeti au nguo kama godoro. Kwa amkubaliano maalum Kliniki ya Mifugo ya SUA inaweza kukupatia chombo maalum cha kubebea Paka anapohitaji kuletwa hospitali.
.

PAKA ANAPOUGUA

Paka wako anapoumwa mjulishe Daktari, usijaribu kumtibu wewe mwenyewe au mtu asiye na ujuzi, kwani paka ni rahisi sana kudhurika kutokana na matumizi mabaya ya madawa, hata kama dawa hizo haziwadhuru wanyama wengine.

Kwenye dharura kama vile, paka akizimia, anapokua dhaifu ghafla, anapovuja damu kwa wingi, kushindwa kupumua, anapotapika mfululizo, au kuhara kusikokoma toa taarifa haraka kwa Daktari.

CHANJO DHIDI YA MAGONJWA

Paka (hasa wa paka wadogo) huathiriwa sana na magonjwa ya virusi. Paka pia huwa wanaugua kichaa cha mbwa na huweza kuuma binadamu kama mbwa afanyavyo. Wasiliana na daktari juu ya chanjo anazoweza kumpa paka wako. Tafadhali muulize daktari maswali kuhusu suala lolote linalohusu mnyama wako. Usingoje mpaka paka wako anaumwa ndio utafute ushauri.

MINYOO.

Pamoja na kushughulikia afya ya paka kwa ujumla, kumpa paka dawa za kuua minyoo ni muhimu sana, hasa minyoo ya mviringo (michango), hasa pale paka anapocheza sana na watoto.

Tegu (tape worms) inaweza pia kuwa tatizo muda Fulani. Kama paka anategu, vipande vyake vinaweza kuonekana sehemu ya mkiani kama punje za mchele ambazo mara nyingine huonekana vikitembea. Kuna aina za tegu ambazo humpata paka kwa kula panya au viroboto, na hivyo kufanya udhibiti wa viroboto uwe na umuhimu wake.

Kwa paka wakubwa, kuwapa dawa kila miezi 6 inatosha, lakini unaweza kuwapa dawa za kuua minyoo kabla ya miezi 6 ikiwa minyoo itaonekana kwenye kinyesi. Paka wadogo wapewe dawa kila baada ya miezi mitatu.

Kuna aina nyingi za dawa zinazotibu minyoo ya paka. Fika kliniki upate ushauri wa dawa zinazofaa kwa mazingira ya hapa Morogoro.

VIROBOTO.

Paka huweza kupata viroboto bila kuonyesha dalili, lakini mara nyingi paka wenye viroboto hujilamba, kujikuna na hata kujiuma hasa mgongoni na kwenye mkia. Baadhi ya paka huathirika pale ngozi inapokutana na mate ya viroboto, hivyo kuumwa na kiroboto mmoja tu huweza kupelekea kuwashwa sana hata kutoka manyoya. Viroboto huweza kuonekana kama vitu vidogo vya kahawia vinavyotembea kwenye manyoya ya paka, au uchafu kwenye manyoya.

Fika kliniki kwa ushauri juu ya kudhibiti viroboto ikiwa ni pamoja na aina ya dawa na jinsi ya kutumia. Daima fuata maelekezo na hakikisha wanyama wengine nyumbani hawana viroboto.

Mara utakapoona viroboto kwa paka wako, tumia dawa pia katika mazingira ambamo paka hukaa. Hii ni kwa sababu viroboto hutumia muda mwingi katika maisha yao kukaa kwenye mazingira, na huenda kwa mnyama kunyonya damu tu. Ondoa matandiko na yasafishe kwa maji ya moto, kazi hii pia ihusishe boksi au kapu la kubebea paka. Madawa ya kunyunyiza ya kuua wadudu pia yanaweza kutumika kwenye kapeti na samani.